



# **KIBABII UNIVERSITY**

## **UNIVERSITY EXAMINATIONS**

**2022/2023 ACADEMIC YEAR  
FIRST YEAR SECOND SEMESTER  
MAIN EXAMINATION**

**FOR THE DEGREE OF MASTER OF ARTS IN KISWAHILI**

**COURSE CODE: SWA 824**

**COURSE TITLE: UPEO WA USHAIRI WA KISWAHILI**

**DATE: 26/4/2023**

**TIME: 2-5 PM**

### **MAELEKEZO**

Jibu maswali **matatu** pekee.

Usiandike chochote kwenye karatasi hii ya maswali

**MUDA: Saa Tatu (3)**

**KIBU** observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

## Maswali

1. a) Fafanua dhana ya ushairi kama inavyopambanuliwa na wataalam mbalimbali kwa kuzingatia mitazamo ya kimapokeo na kiusasa. (alama 8)
- b) Soma shairi la “Ukubwa Jaa” (Wallah, 1988) kisha ueleze bahari, umbo, idhini ya mshairi na matumizi ya lugha. (alama 12)

### **Ukubwa Jaa**

Dunia yetu dunia, watu wanakufitini  
Dunia huna udhia, watu wanakulaani  
Dunia huna hatia, wabebeshwa kila zani  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia umenyamaza, umetua kwa makini  
Dunia vitu mejaza, watu wanataka nini?  
Dunia wanakuchezea, binadamu maliuni  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia mtu akose, hukutia mdomoni  
Dunia hebu waase, hao watu mafatani  
Dunia chuki mpuse, muipate afueni  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia una lawama, za uongo si yakini  
Dunia wanokusema, ni manjunju si razini  
Dunia huna hasama, waja ndio kisirani  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia kuharibika, hayo amezusha nani?  
Dunia watu humaka, hao wanaokuhini  
Dunia umejazika, kila tunu ya thamani  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia unatulisha, bwerere bila undani  
Dunia unatukosha, maji tele baharini  
Dunia unaotesha, mimea tosha shambani  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia hujageuka, tangu uumbwe na Manani  
Dunia watu ndo nyoka, mahaini na wahuni  
Dunia una baraka, mwenye pupa hazioni  
Dunia huna ubaya, wabaya ni insani!

2. Pambanua nadharia moja moja za uchambuzi wa mashairi ya kijadi na kisasa huku ukionesha matumizi yake katika mifano ya mashairi kutoka diwani mbili za ushairi ulizosoma katika kozi hii. (alama 20)
3. Fafanua sababu zilizopelekea kuzuka kwa mgogoro katika ushairi wa Kiswahili miaka ya 1970. (alama 20)
4. Dadavua kwa kutoa mifano, sifa bainifu za ushairi katika kipindi cha urasimi mkongwe. (alama 20)
5. a) Kwa kutumia mifano, eleza dhana ya mashairi ya mijini. (alama 4)  
b) Pambanua sababu tano za kimsingi wanazotaja wataalam wa ushairi zinazopelekea wapenzi wa ushairi kuyachangamkia mashairi ya mijini. (alama 10)  
c) Fafanua sababu zozote tatu za juhudi za wasawazishaji za kuwapatanisha wanamapokeo na wanamapinduzi. (alama 6)